# Dhana ya Utendaji na Dhima Yake katika Tamthilia ya *Kitumbua Kimengia Mchanga*

*Jackson Ndung'u Mwangi*
*Chuo Kikuu cha cha KCA*

**Ikisiri**

**Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya utendaji iliyoasisiwa na Wallace Bacon ili kubainisha ikiwa tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* iliyoandikwa na Mohamed (2000) imezingatia kigezo kikuu katika matini za kidrama ambacho ni uwezo wa kuwasilishwa jukwaani au ni majibizano ya usemi tu. Katika utafiti huu tumevitathmini vipengele vinavyochochea na kufanikisha utendaji wa tamthilia kwenye jukwaa. Maelekezo ya jukwaa, mandhari, maleba, miondoko, sauti, uangazaji, kimya na mihimili ni vipengele vya utendaji ambavyo huwawezesha waigizaji kuwasilisha ujumbe wa mwandishi kwenye jukwaa. Utafiti huu umejaribu kubainisha jinsi vipengele hivi vinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa na pia kutaja kwa ufupi dhima zinazofungamana na matumizi ya vipengele hivi. Utafiti huu ulihusisha kusoma makala na kutumiwa kama data ya utafiti huu ambayo baadaye ilichanganuliwa na mwishowe kuelezea matokeo kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Utafiti huu pia ulihusisha ukusanyaji wa data moja kwa moja kutoka maktabani. Mahali pa utafiti palikuwa ni maktaba katika vyuo vikuu pamoja na maktaba ya kitaifa nchini Kenya na kundi lengwa lilikuwa tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Inatarajiwa kuwa utafiti huu utakuwa mchango mkubwa kwa jamii ya wasomi hasa wanaoshughulikia utendaji na vipengele vya kidrama katika fasihi andishi.**

**Maneno Muhimu**: Utendaji, Tamthilia, Nadharia ya Utendaji, Drama, Vipengele vya Utendaji.

**Utangulizi**

Kimsingi, tamthilia huandikwa kama hadithi fupi ya kuwasilishwa jukwaani. Licha ya kuwa tunaweza kuisoma tamthilia, ukamilifu wake ni katika kuitazama inapoigizwa jukwaani. Ni kwa sababu hii ambapo pana umuhimu mkubwa wa kuvichunguza vipengele vinavyohusika katika kulifanikisha jambo hili kwani uhusiano uliopo baina ya kazi yenyewe na hadhira una mguso zaidi kwa kuwepo waigizaji wanaoonekana.

Utafiti huu ulihusu utendaji katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* iliyoandikwa na Mohamed (2000). Utafiti wetu umejikita katika kuchanganua tamthilia hii na kutathmini kuwepo kwa vipengele vya utendaji ambavyo huzipa tamthilia hadhi ya kuwa matini za kidrama. Vipengele hivi huziwezesha tamthilia kuwasilisha ujumbe kwa njia ya uigizaji kwenye jukwaa.

Utendaji ni neno linalotokana na kitenzi tenda. Istilahi hii inahusishwa na sanaa za maonyesho na huhusisha uwasilishaji wa igizo fulani mbele ya hadhira. Mkazo wake mkubwa upo kwenye vitendo. Kuhusu utendaji katika fasihi, waandishi Madison na Hamera (2005) wanaeleza kuwa utendaji na fasihi una uhusiano wa karibu. Utendaji ni njia tunayoitumia kuingia katika ulimwengu wa fasihi. Utendaji una midundo mingi (*polyrhymic*) kwani unaunganisha maneno, tajriba, hulka, udhanifu, mwili wa msomaji na matini ya kifasihi. Kulingana nao, suala la utendaji ni dhana tatanishi na changamano mno.

Wamitila (2003) anasema kuwa matendo ya wahusika hudhihirika kupitia kwa utendaji kwenye jukwaa au vionekanavyo jukwaani, kitu ambacho kinachukuliwa kuwa mhimili wa tendo fulani. Katika kazi yake ya 2008, mwandishi huyu anasema kuwa drama huwasilisha hadithi kama ilivyo katika riwaya au hadithi fupi ila tu hii huwasilishwa kwa mtindo wa mazungumzo ambao unadhamiriwa kuwasilishwa au kuonyeshwa jukwaani na waigizaji kwa kuzingatia kaida fulani za kimsingi za drama. Vilevile, katika kazi hii Wamitila (2008) akimnukuu Were (2012) anaeleza kuwa

drama hurejelea sanaa za maonyesho au maigizo. Kulingana naye, fasili hii inaelekea kupuuza kuwa drama aghalabu hurejelea matini iliyoandikwa kwa maneno yanayohusishwa na wahusika wanaopatikana katika matini. Kulingana naye, drama haishii kwenye utunzi tu bali pia huhusisha masuala yanayofungamana na uigizaji, uangazaji wa jukwaa, mitagusano ya waelekezi, maleba na muziki. Kwa msingi huu ni rahisi kusema drama inaanza tu baada ya kuandikwa tofauti na riwaya inayoisha tu iandikwapo. Mwanadrama anaweza kuwasiliana na hadhira kupitia kwa wahusika wake. Maoni ya wataalamu hawa bila shaka yanaafikiana hasa kuhusu umuhimu wa vipengele vinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa tamthilia kwenye jukwaa.

Kwa jumla, tamthilia ni utanzu ambao hutegemea mazungumzo na uigizaji ili kuwasilisha ujumbe wake. Hii ni kwa sababu njia inayomwezesha msanii kuwasilisha wazo lake vyema ndiyo mwafaka. Nguzo kuu ya kazi hii ni utendaji kwani matendo ya wahusika hudhihirika kupitia utendaji katika jukwaa. Hivyo basi, bila shaka kipengele cha utendaji kinachukua nafasi muhimu katika tamthilia. Ni katika msingi huu ndipo tatizo la utafiti huu ni kuchunguza ikiwa tamthilia ya *Kitumbua Kimeinguia Mchanga* inaweza kudai nafasi yake kama matini ya kidrama. inaweza kudai nafasi hii kwa kubainisha mambo yanayochochea uigizaji. Mambo haya ni maelekezo ya jukwaa, mandhari, uangazaji, maleba, miondoko, sauti, mpangilio wa jukwaa, nje ya jukwaa, kimya, vifuasi vya maleba na mihimili kama yalivyoorodheshwa na Nadharia ya utendaji iliyoasisiwa na Wallace Bacon (1984) na kuendelezwa na Grifffiths na Heming (1984) Pamoja na Wamitila (2008).

Uhakiki wa tamthilia umefanywa na umeshughulikia mambo mbalimbali kama vile: nafasi ya tamthilia za kihistoria, taswira ya mwanamke, msimbo na maana kwa kuzingatia nadharia ya semiotiki, michango ya vijana kama watu wachanga waliokengeuka na kupotoka. Uhakiki huu wa awali haukuangazia uhusiano kati ya matini na utendaji ili kubainisha ikiwa watunzi husika wamezingatia vigezo au mambo ya kimsingi yanayochochea utendaji katika matini za kidrama. Utafiti huu umeamua kuvishughulikia vipengele hivi vinavyochochea na kufanikisha uigizaji.

Utafiti huu ulioongozwa na Nadharia ya Utendaji katika kuchanganua matini za kidrama na kubainisha ikiwa tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* imezingatia kigezo kikuu ambacho ni uwezo wa kuwasilishwa jukwaani au ni majibizano ya usemi tu.

Kulingana na Madison na Hamera (2005) mwasisi wa nadharia ya utendaji ni Wallace mwaka wa 1984. Alifafanua utendaji wa kifasihi kama tendo lenye msingi wake katika kuleta msisimko miongoni mwa waigizaji na hadhira. Hii ni kupitia kuifanya hai stadi hii ya kifasihi kupitia uangazaji wa uwingine na wengine (otherness and others) na kuvuka mipaka ya umimi. Kwake yeye, kuungana kwa stadi ya kufasiri matini ya kifasihi ni kuvuka mipaka ya umimi ya msomaji wa tamthilia. Alisisitiza kuwa kitovu cha utendaji ni mtagusano kati ya wasomaji na matini, jambo linalostawisha kuendeleza, kubainisha na kubadilisha maisha ya ndani ya waigizaji na pia hadhira. Kwake Wallace msomaji wa tamthilia hunufaika yeye binafsi kutokana na ujumbe lakini katika uigizaji kwenye jukwaa idadi kubwa ya hadhira hunufaika kutokana na ujumbe. Tamthilia inapoigizwa katika jukwaa ujumbe huwafaidi na kuwafikia wengi na sio msomaji pekee. Madison na Hamera wanasema kuwa Wallace aliongeza na kupanua stadi ya kusoma na kukariri usemi hadharani na kufanikisha uwezo wa kufasiri na kuigiza matini ya kifasihi mbele ya hadhira.

Wallace (1984) anaendelea kudai kuwa hadhira kubwa hunufaika kutokana na uigizaji, hivyo basi nadharia ya utendaji inafaa katika kuvitathmini vipengele vinavyofanikisha na kuleta ukamilifu katika uigizaji. Baadhi ya mihimili na vipengele vya utendaji na drama vilivyoorodheshwa kwa mujibu wa nadharia hii ni maelekezo ya jukwaa, mandhari, uangazaji, maleba, miondoko, sauti, mpangilio wa jukwaa, nje ya jukwaa, kimya, vifuasi vya maleba na mihimili.

Hivyo basi nadharia ya utendaji inashughulikia kuifanya hai fasihi. Ni vigumu kufanya hivyo bila kuhusisha vipengele vinavyochochea utendaji. Ndipo utafiti huu umeamua kutumia nadharia hii ya utendaji kuhakiki utendaji katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga.* Nia ya utafiti huu ni kutathmini ikiwa vipengele vya utendaji vinajitokeza katika kazi hii. Ni lengo la mtafiti pia kutathimini ikiwa tamthilia hii inaweza kudai nafasi kama matini ya kidrama kwa kuvizingatia vipengele vinavyochochea utendaji kwenye jukwaa. Mtafiti alizingatia nguzo sita za nadharia hii

katika kufanikisha utafiti wake ambazo ni: mandhari, maleba, miondoka, uangazaji, sauti, kimya na mihimili. Griffiths na Hemming (1984) wameziita sifa hizi zinazofanikisha uigizaji ishara za kidrama nazo ni mpangilio wa jukwaa, mandhari, miondoko, viashiria, maleba, maelezo kwa hadhira, muziki, uangazaji, maelekezo ya jukwaa na kimya. Vipengele hivi ni mwafaka katika utafiti huu kwa sababu ndivyo vitakavyochanganuliwa na sifa zake kuwekwa wazi.

Auslander (2008) anasisitiza kuwa drama au kazi ya maigizo huandikwa kimsingi ili iwasilishwe mbele ya hadhira. Kulingana naye, hali hii inatukumbusha kuwa ni muhimu tunapozichunguza matini za kidrama kuangazia ikiwa zina unyumbufu wa kiasi gani. Kutokana na sifa ya uhai inayohusishwa na kazi hii, sifa muhimu zinazorejelewa ni: jukwaa, ishara za mikono, lugha, toni na maneno ya wahusika, ishara uso, mbinu za ubainishaji na ukuzaji wa wahusika, mazingira, upodoaji, maleba, uangazaji, sauti, nyimbo, muziki na ngoma. Kazi hii ni mwafaka kwetu kwa sababu imedokeza vipengele vinavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwenye jukwaa. Tofauti ni kwamba utafiti huu haushughulikii toni ya maneno ya wahusika, ubainishaji na ukuzaji wa wahusika na upodoaji.

Were (2012) amechunguza fani katika tamthilia ya Kiswahili huku akirejelea tamthilia za *Kilio cha Haki* na *Kijiba cha Moyo*. Mhakiki huyu amechanganua vipengele vinne vya fani ambavyo ni ploti, wahusika, dayalojia, na monolojia kwa kuonyesha jinsi vinavyojenga kazi nzima. Uhakiki huu unashughulikia vipengele vinavyowawezesha wahusika kudhihirisha hisia zinazotokana na ishara za nyuso zao wanapozungumza jukwaani na hivyo basi kazi hii ni mwafaka katika uchanganuzi huu kwani unashughulikia suala la uigizaji katika tamthilia.

Utafiti huu unahusu vipengele vinavyofanikisha uigizwaji katika tamthilia. Ili kutekeleza utafiti huu, mtafiti alijikita katika kusoma tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* ili kutathmini vipengele vinavyofanikisha utendaji kwenye jukwaa. Katika maktaba mtafiti alisoma kazi zinazohusiana na mada hasa zinazogusia vipengele vya utendaji katika fasihi hasa katika tamthilia. Vilevile, mtafiti alirejelea mtandao kutafuta habari mwafaka zinazohusiana na Nadharia ya Utendaji katika fasihi. Isitoshe, mtafiti alirejelea kamusi maalum za fasihi pia ili kuweza kubainisha vipengele vinavyohusiana na utendaji. Pia, Mtafiti alizungumza na wataalamu wanaofundisha drama na amezisoma matini zingine za kidrama ili apate msingi thabiti wa kuzitathmini tamthilia husika.

## Uchambuzi wa Vipengele Muhimu vya Utendaji katika Tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*

### Maelekezo ya Jukwaa

Mbatia (2001) anaeleza kuwa haya ni maelezo katika tamthilia ambayo huwa yameandikwa kwa hati mlazo na kuwekwa kwenye mabano juu ya miondoko ya wahusika, matendo yao na ishara wanazofanya. Maelezo kama haya pia yanatoa picha ya mandhari ya jukwaa. Kwa ujumla, maelekezo haya hutoa maelezo kuhusu mienendo na miondoko ya wahusika, hutoa maelezo kuhusu wasifu wa wahusika kama vile mavazi, lugha na ishara uso. Pia, hutoa maelezo kuhusu mandhari au mahali pa mchezo, hufafanua mazingira na hata maleba ya wahusika. Vile vile, hutoa vielekezi vya jinsi ya kuandaa jukwaa kwa ajili ya uigizaji. Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, mtunzi ametumia maelekezo ya jukwaa kudokeza mandhari, maleba, uangazaji, miondoko, sauti, mihimili na kimya.

### Mandhari

Mbatia (2001) anasema kuwa istilahi hii inahusiana hasa na utanzu wa drama na inarejelea sura mahsusi inayotokana na mapambo na vifaa vilivyopangwa kwenye jukwaa. Sura hiyo huwa imedhamiriwa kuiga mazingira halisi yaliyoelezwa katika tamthilia inayoigizwa. Mazingira kama hayo yanaweza kuwa nyumbani, njiani au kwenye uwanja wa vita. Pia anasema kuwa mandhari hutumiwa kwa maana ya sura ya mahali, hasa ikiwa ya kuvutia. Kwa mujibu wa tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga*, mtunzi amefanikisha dhana hii na kuibua dhima mbalimbali. Kwa mfano:

> **1. [***Magharibi.***Ukumbini** *mwa Bw. Mambo mwenye umri wa miaka 50 na Bi Sikitu mwenye umri wa miaka 45.* ***Ukumbi mzuri mwenye samani ya fahari inayothibitisha uwezo wa***

***kiuchumi**. Angia Bi Haja, mamake Bw. Mambo mwenye umri wa miaka 70 hivi. Mkono wa kushoto amebeba sahani na kawa, anagonga kwa mkono wa kulia.]uk 3.*

Katika onyesha hili, maelezo haya yanamwelekeza msomaji katika kutambua ni wapi onyesho husika linaanzia. Mtunzi ametambulisha kuwa matukio katika onyesho hili yanatukia ukumbini katika makazi ya Bw. Mambo. Mandhari haya pia yanatambulisha kuwa yanatendeka wakati wa magharibi na yanathihirisha uwezo wao wa kiuchumi.

Katika onyesho hili pia, mtunzi anaendelea kutambulisha mandhari mbalimbali kama vile

**2.** *[**Ukumbini** palepale. Fatuma na Bi. Sikitu wanaweka vyakula mezani. Bwana mambo aliyevaa miwani amekaa katika sofa anasoma gazeti… Wote ndio kwanza wamerudi kutoka **msikitini** kwa sala ya magharibi na sasa wanangojea chajio.] uk. 15*

Katika onyesho hili, mandhari haya yanampa msomaji fununi zaidi kuhusu makazi na maisha ya familia ya Bw. Mambo. Ilikuwa ni wakati wa jioni baada ya Bw Mambo, Fikirini, Baddi na rafikiye Fikirini, Faki walipotoka msikitini kwa sala. Hapa, inabainika wazi kuwa walikuwa wacha Mungu na walikuwa wakishiriki dini ya Kiislamu. Isitoshe, inatambulika kuwa wanawake kamwe hawaandamani na wanaume kwenda sala wakati wa magharibi. Mandhari haya pia yanadokeza nafasi ya mwanamke katika jamii. Kwa mfano, mwanamke ana jukumu la kuiandalia aila yake vyakula.

**3.** *[**Ukumbini** mwa Bi. Haja. Kuna **samani za dhamani ya juu**: sehemu ya maonyesho ya mafanikio ya mwanawe. Tunamkuta Bw. Mambo kaketi juu ya sofa la sifa na mama yake Bi. Haja, sofa la pili mkabala naye. Juu ya meza ya kimo cha wastani, baina yao pana vileja, kashata za mayai na vitumbua… uk 23]*

Mandhari haya yanayopatikana nyumbani kwa Bi. Haja yanadhihirisha kuwa Bi. Haja ambaye ni mamake Bw. Mambo aliishi maisha ya kifahari.

Kwa ujumla, mandhari katika tamthilia hii yana umuhimu wa kumdokezea msomaji kuhusu pale ambapo matukio yanatukia, yanatukia saa ngapi na hali za maisha za wahusika wanaotekeleza majukumu anuwai katika tamthilia hii.

**Maleba**

Wilson (1998) anadai kuwa maleba ndicho kipengele cha kipekee cha vitu vionekanavyo katika jukwaa. Waigizaji na maleba huchukuliwa kama kitu kimoja, huungana na huwa sura moja katika jukwaa. Vilevile maleba yana thamani ya kipekee. Huongeza kipima rangi, umbo, msokotano na uashiriaji kwa athari nzima. Maleba yana uhusiano wa karibu na vifuasi kama vile vipodozi, mapambo ya mwili kama vile mikufu na bangili, mitindo ya nywele, mafigu na nywele bandia. Maleba yana uwezo wa kuwasilisha ujumbe mzito kwa hadhira fauka ya kupendeza. Suala hili linabainika katika onyesho la pili.

**4**. [*Ukumbini pale, Fatuma na Bi Sikitu wanaweka vyakula mezani. Bw. Mambo **aliyevaa miwani** amekaa katika sofa anasoma gazeti…] uk 15.*

Katika muktadha huu, miwani iliyovaliwa na Bwana Mambo inatumika kama maleba. Miwani hii inadhirisha uwezo wa Bwana Mambo wa kuwa na mali nyingi na inaonyesha tabaka la watu katika jamii wenye uwezo wa kifedha. Katika onyesho hili pia, Bwana Mambo anatumia miwani kuwaangalia Faki na Fikirini kwa kejeli wanapojadili maswala tata yanayopatikana katika kitabu cha fasihi walichokuwa wakikichambua kilichoandikwa na mwandsihi Zanga. baadaye, inabainika wazi kuwa uozo waliokuwa wakichambua Fikirini na Faki uliendelezwa na Bw. Mambo.

**5.** [*Katika chumba cha Fikirini. Ni chumba cha fahari. Fikirini yupo kitandani akisema na kitabu chake mikononi. **Kavaa kisuruali kipande kinachomfika mapajani**. Bi. Sikitu anagonga mlango wa chumba hicho akimwita mwanawe*…]

Katika onyesho hili, Fikirini anaonekana kuvaa kipande cha kisuruali kinachomfika mapajani. Hii inaonyesha kuwa licha ya yeye kutoka kwenye familia iliyojiweza, fikra zake hazijaingiwa na kasumba walizo nazo matajiri wengi za kuvaa mavazi ya dhamani kubwa ila yeye anaishi maisha ya

kawaida tu kama wenzake. Isitoshe, hali ya Fikirini kuvaa kipande cha kisuruali inaondoa urasmi katika uwasilishaji wa tamthilia hii na kusawiri ya maisha ya kawaida mtu akiwa nyumbani.

**Miondoko**

Griffiths na Hemming (1984: 104) wanaeleza kuwa hali ya kuonekana ya drama katika jukwaa huwezesha miondoko kuwa na athari kubwa. Wahusika huweza kusonga kwa ustadi hadi neno lililosemwa likastawishwa au kimya kikajazwa maana. Msomaji wa drama mwenye tajriba na makini atabuni miondoko yake. Lakini hata msomaji asiye na tajriba ni sharti atambue maelezo mahsusi ya miondoko yaliyotolewa katika maelekezo ya jukwaa. Wasifu, tabia na saikolojia za wahusika huonekena katika utendaji. Hivyo basi, ni sharti pawe na ubunifu mkubwa wa miondoko ambayo husaidia kuweka wazi mambo hayo wakati wa utendaji. Kwa mujibu wa tamthilia hii, miondoko mbalimbali imebainika.

> **6.** *[ Magharibi. Ukumbini mwa Bw. Mambo mwenye umri wa miaka 50 na Bi. Sikitu, mwenye umri wa miaka 45. Ukumbi mzuri wenye samani za kifahari inayothibitisha uwezo wao wa kiuchumi.* ***Aingia Bi. Haja****, mama wa Bw. Mambo mwenye umri wa miaka 70 hivi. Mkono wa kushoto umebeba sahani na kawa. Anagonga kwa mkono wa kulia.]*

Katika onyesho hili, miondoko ya Bi. Haja inabainika waziwazi wakati anaingia katika makazi ya Bw. Mambo. Kuingia kwa Bi. Haja katika makazi haya kunampa msomaji fununu kuhusu uhusiano wake na Bw. Mambo. Inabainika wana uhusiano wa karibu hivi kwamba Bi. Haja ni mamake Bw. Mambo hii ni kutokana na hali ya kuwajibika kwake kwani anawaletea kahawa na vitumbua.

> **7.** [BI. MWATIMA...*Nimekikuta hicho ki-Hidaya…mhn; a-a [****anapiga kofi****] dunia imeharibikia. Shoti anapita akicharaza njiani, kahazinika sauti, kifua mbele, madodo pwa-pwa-pwa yasiyotiwa vikapuni…[* ***anasimama kwa kupepesuka kumwiga Hidaya alivyokuwa akienda huku madodo yakidunda; kisha anarudi kuketi palepale sofani.****] Uk 19.*

Katika sura hii, swala la miondoko linadhihirika pale ambapo Bi. Mwatima anaingia kwa Bw. Mambo huku akieneza uvumi kuhusu yale aliyoyasikia kumhusu Hidaya. Hii ni kwa sababu inadaiwa Hidaya alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na vijana wa mtaani. Anaanzisha umbea huu kwa kupiga makofi ili kuteka fikra za wawili hawa (Bw. Mambo na Bi. Sikitu). Bi. Mwatima anaendeleza miondoko kwa kuiga vile ambavyo Hidaya hutembea akiwa katikati ya vijana bila woga wowote. Anasimama na kutembea kwa madaha kifua kikiwa mbele na madodo yakimdunda. Miondoko hii inadhihirisha jinsi wanawake wanavyoendeleza uvumi dhidi ya wanawake wenzao. Pia, inabua sifa tabia za Bi. Mwatima za kueneza umbea kutokana na mambo ambayo bado hajayadhibitisha.

> **8**. [*…****Aingia Bi. Sikitu kutoka chumbani na kujitupa sofani huku akilia****. Analia kwa kelele, kwikwi na hamsa… aingia Fatuma kutoka ndani kuja kumshika mama yake mabega ili kumnyamazisha…*].

Katika onyesho hili, miondoko inadhihirika pale ambapo Bi. Sikitu anaingia na kuanza kulia kutokana na madhila anayopitia Fikirini. Hii ni kutokana na hali kuwa Bw. Mambo amekataa Fikirini kujichagulia mke kwani anataka amchagulie yeye. Anapoendelea kulia, Fatuma anaingia na kuanza kumtuliza mamaye, jambo linalodhihirisha kuwa wanawake pia wanawajali wanawake wenzao. Miondoko hii inazaa matunda kwani baadaye kabisa, Bw. Mambo analegeza masimamo wake na kumwachilia Fikirini kumwoa Hidaya, jambo linalodhihirika wazi kuwa wanawake wana ushawishi mwingi kwa waume wao.

Mtunzi wa tamthilia hii ameitumia stadi ya miondoko kwa upana na kwa njia ambayo imefanikisha uigizaji. Amebainisha miondoko ya mwili na viungo vyote vya mwili vikitumika kubainisha hisia mbalimbali.

**Uangazaji**

Mwangaza huiwezesha hadhira kuona vyema waigizaji na matendo yao. Uangazaji huongeza umuhimu katika utendaji na kutuelekeza kwenye athari maalum. Wamitila (2011) ameeleza kuwa uangazaji wa jukwaa ni muhimu katika uigizaji. Taa hutumiwa kulimulika eneo walipo wahusika

wanaotenda tendo fulani. Taa hizi huweza kutumiwa kwa namna ambayo inazua picha fulani. Kwa mfano, taa nyekundu kuonyesha hatari, giza kuonyesha uovu au ukosefu wa mwelekeo na taa hafifu kuonyesha kukosa uhakika au msimamo. Uangazaji hivyo basi una uwezo wa kuzua hisia za furaha, masikitiko na hata hasira. Katika kazi ya uigizaji, mazaji hujitokeza vyema jukwaani kuliko katika maandishi.

Matumizi ya kipengele hiki pia yamechunguzwa katika tamthilia ya *Kitumbua Kimengia Mchanga*.

**9.** [ *ghafla, inapiga radi na umweso*] uk 41.

Katika onyesho ili, mwangaza wa radi unabainika wakati Bw. Nia anazungumza na Faki pamoja na Fikirini ufuoni wa bahari wakati mawimbi yanapiga. Katika bahari hii pia, inadhihirika wazi kuwa bahari linapiga kwa kasi. Mwanga huu unaotokana na kupiga kwa radi unadhirisha vile maisha ya siku hizi yanavyosonga kwa kasi na jinsi yanavyoathiri setka sote za maisha ikiwemo sekta ya ndoa. Bw. Nia anadai kuwa wazee wanashikilia utamaduni ili kujaribu kukidhi hali mbalimbali za maisha yao lakini mambo ambayo bado wanayashikilia yanapitwa kasi sana na mabadiliko ya kisasa. Kwa hivyo, kulingana na Bw. Nia ambaye ni mzee aliyezinduka licha ya kuwa yeye ni maskini na anafanya kazi ya uvuvi tu, ni vyema wazee waweze kukubali matokeo ya mabadiliko katika maisha yao.

**10.** [*Wanaendelea kurudia usemi huu huu mpaka wote hawaonekani jukwaani na halafu* ***taa ghafla zinazima****. Kwa sekunde fulani, kunakuwa na* ***giza totoro***] uk. 58

Kwa mujibu wa onyesho hili, uangazaji unafifia kwa ghafla na kuwa na giza totoro kumaanisha kuwa wanawake waliokuwa wakiimba nyimbo za kusherehekea harusi wamefikisha kikomo uimbaji wao na pia kuashiria kuwa onyesho limefika mwisho. Pia, kuzima kwa mwangaza huu kunasadia wahusika watakaojihusisha na onyesho kujipanga na kutokea kwenye jukwaa.

**11.** [ ***Taa zinawaka*** *tena kama zamani. Na sasa wanaingia maarusi, Fikirini na Hidaya, ambao wamevalia vyema kiarusi, wakiongoza na kuandamana na wazee wao na Rubaa yao…*] uk 58.

Kuwaka kwa taa hizi kunatanguliza kuwapisha maarusi wanaongia ambao ni Fikirini na Hidaya. Taa hii pia inaashiria kuwa suala la ndoa ni shughuli ambayo ni safi na hali ya kitumbua kuwa safi na kutoingia mchanga kabla ya ndoa ni jambo ambalo linadhaminiwa sana katika jamii hii. Mtunzi wa tamthilia hii amekitumia kipengele hiki cha uangazaji kuiwezesha hadhira kuona yale yanayoigizwa kwenye jukwaa. Giza, mwangaza hafifu na hata mwangaza uliong'aa ni mambo ambayo yametumika kuwasilisha ujumbe wa tamthilia kwa njia mbalimbali.

**Sauti**

Sauti ni kipengele cha utendaji ambacho hakionekani kama vipengele vingine lakini husikika. Siku za hivi karibuni, sauti imekuwa kipengele muhimu cha kithieta kutokana na ubunifu wa kithieta, usanii, teknolojia na usanifu wa kipekee. Njia moja ya kuainisha usanii wa sauti ni kwa sauti iliyobuniwa upya na sauti iliyoimarishwa kulingana na maoni ya Wilson (1998). Sehemu hii inatathmini matumizi ya kipengele hiki cha sauti katika tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga.*

**12.** FAKI [ *Kwa* ***sauti ya chini*** *na huku amekamata kitabu cha mwandishi Zanga*] *uk. 15.*

Katika sehemu hii Faki na Fikirini wanazungumza kwa sauti ya chini kwa chini kuhusiana maswala yaliyomo katika kitabu cha mwandishi Zanga. Sababu yao kuzungumza kwa sauti ya chini ni kwa sababu kulikuwepo na wahusika wengine kule ukumbini kama vile Bw. Mambo aliyekuwa akisoma gazeti hivyo iliwafaa wasipige kelele wakati ule. Pia, kushauriana kwao kwa sauti ya chini kwa chini kuna umuhimu kwani kungefanya uchambuzi na uhakiki wao wa fasihi uzame akilini mwao kwa njia inayofaa. Isitoshe, mazungumzo haya yanabainisha usuhuba waliokuwa nao wawili hawa na uhusiano wa kimasomo na kififikra waliokuwa nao.

**13.** [ ***Hodi mlangoni****… Aingia B. Tukaije na* ***kilio****. Anajitupa sofani…*] uk. 8.

Sauti hii inaonyesha kuwa Bi. Tukaije ameingia katika makazi ya Bi. Sikitu baada ya kubisha hodi mlangoni. Pia, sauti inayotambulika katika kilio cha Bi. Tukaije inaibua taharuki kwa Bi. Sikitu na kumwacha akijiuliza kunani katika maisha ya Bi. Tukaje. Pia, kilio hiki kinamwacha msomaji na taharuki ya kutaka kujua ni nini kilichosababisha kilio hiki na kitaisha lini.

**14.** BI. TUKAIJE: [***Sauti yake bado imo katika kilio***] *uk.9*

Hata baada ya Bi. Tukaije kutulizwa na kuliwazwa na Bi. Sikitu, Bi. Tukaije anaamua kumjibu lakini sauti yake imejaa kilio. Bi. Tukaije anajaribu kumweleza Bi. Sikitu kuwa kilio chake kinatokana na jinsi hali ya malezi imekuwa ngumu kutokana na mpito wa wakati. Anadai kuwa kulea watoto husasan wa kike kuna changamoto kubwa sana kwani wanapata mimba za mapema kila uchao na kuathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya.

**15.** [ ***Simu ya inalia*** *na Bw. Mambo aliye karibu nayo anaipokea*].

Sauti ya simu hii ya Bw. Mambo inapolia, inakatiza mjadala kati yake na akina Fikirini kwamba fasihi haina umuhimu katika maisha ila kilicho na umuhimu ni masomo yanayohusiana na biashara na uchumi. Pia, mlio wa simu unampa msomaji fufunu kuhusu uwezo wa kifedha alio nao Bw. Mambo. Isitoshe, mawasiliano yanayobainika baada ya Bw. Mambo kuchukua simu yanadhirisha jinsi anavyojiingiza katika ufisadi, magendo na biashara ya uuzaji dawa za kulevya.

**Kimya**

Griffiths na Hemming (1984) wanasema kuwa uzingativu wa hadhira unavutiwa zaidi na maneno au miondoko. Mhusika anayezungumza huenda akashughulisha macho na masikio. Ikiwa mhusika bubu aliye kimya ataingia au atatenda mwondoko wazi, yeye atavuta mawazo. Kimya kinaweza kuwa na umuhimu sana. Wakati wa kusoma tamthilia kila mara husaidia katika kukumbuka nani yuko katika jukwaa na hazungumzi. Katika tamthilia ya *Kitumbua Kimengia Mchanga,* swala hili linadhihirika kutokana na mifano ifuatayo.

**16. BI HAJA**: Mnh [*anaguna! Halafu* ***kimya****. Anajitupa sofani kisha anamtumbulia macho Bi. Sikitu*] *msidhamini ladha ya vyakula tu; mdhamini na nguvu za mapishi pia.) uk.* 4

Kimya hiki kinaendelezwa na Bi. Haja anapozungumza na Bi Sikitu, anapowatembelea kwa Bw. Mambo. Kimya hiki kinadhihirisha jinsi Bi. Haja alivyoudhika kutokana na hatua ya familia ya Bw. Mambo na Bi. Sikitu kuamua kumwacha Fikirini ajichagulie mke aitwaye Hidaya ambaye ni maskini na ambaye ananuiwa kuwa kimetumbua chake kimeingia mchanga baada ya kupatikana akitembea na wanaume ovyo ovyo. Kimya hiki pia kinaonyesha jinsi Bi. Haja anavyopigwa na butwaa kutokana na jinsi ulimwengu wa kisasa unavyobadilika na kuwaathiri watoto wao.

**17. BI. SIKITU**: [ *Anamtazama kwa mshangao na wasiwasi Bi. Haja akitoka*] karibuuu. karibu mama! [***kimya*** *baada ya kuondoka Bi. Haja halafu anasema peke yake*] uk.5.

Kimya hiki kinadhihirika baada ya Bi. Haja kuondoko na kumwacha Bi. Sikitu akiwazia aliloelezwa na Bi. Haja. Kimya hiki kinabainisha mawazo aliyo nayo Bi. Sikitu baada ya kuwachiwa fumbo na Bi. Haja, anajaribu kuwazia fumbo hilo linalohusu kazi ngumu ya utayarishaji wa vitumbua. Analalama pia kuwa Bi. Haja (mama mkwe) haoni lililo njema kwao, ila kila wakati anawakashifu tu. Katika onyesho hili la kwanza pia, kuna kimya kingine ambacho kinadhihirika.

**18.** BI. SIKITU: [***Kimya****; bado Bi. Sikitu amemwekea mwenzake mkono wa kumpozesha begani. Ghafla, Bi. Tukaije anafuta machozi na kuzuka na kigelegele na Bi. Sikitu akijua kigelegelee hicho ni nini…*].

Kimya hiki kinadhirika wakati ambapo Bi. Sikitu anatembelewa na rafiki yake Bi. Tukaije ambaye pia ni jirani yake. Anapofika na kuingia kwa Bi. Sikitu, anaonekana akilia tu bila kusema lolote. Baada ya kimya kifupi, kilio kile kinabadilika na kuwa furaha. Hii ni kutokana na rai kwamba Bi. Tukaije anafurahi kwani msichana wake amefikia umri wa kuolewa na ametafutiwa mchumba bila ya kuharibiwa na mabadiliko yanayodhihirika katika jamii hii ambayo yanawaathiri vijana. Mabadiliko

haya ni kama vile ndoa za mapema, kuavya mimba, kutumia dawa za kulevya pamoja na vijana kushiriki ngono wakiwa wachanga.

**Mihimili**

Kwa maoni ya Griffiths na Hemming (1984), mihimili huchangia ufahamu wa yanayoonekana. Vifaa vyenye maumbo yanayoonekana ni muhimu sana hasa katika kuzua utani au mchezo wa kuchekesha. Mtunzi wa tamthilia hii amethihirisha matumizi ya anuwai ya mihimili.

**19.** [ *Hodi mlangoni… Aingia Bi. Tukaije na kilio. Anajitupa* ***sofani****...]*

Katika onyesho hili sofa imetumika kama mihimili. Sofa hii ina umuhimu wa kipekee kwani inaonyesha jinsi familia ya Bw. Mambo ilivyo na uwezo wa kifedha. Kwa mujibu wa tamthilia hii, sofa pia inaashiria watu wanaoshi maisha ya raha mustarehe. Isitoshe, sofa hii inatumika kama kitulizo au kiliwazo cha moyo. Inabainika waziwazi kuwa Bi. Tukaije alipoingia akiwa analia, anakaa kwenye sofa pale ambapo Bi. Sikitu anamliwaza na kumtuliza na baadaye tunaomwona Bi. Tukaije akiangua kicheka na kudhihirisha furaha.

**20. BI. SIKITU**: Karibu, karibu shoga yangu…keti nikufungulie soda. [*anakwenda kwenye* ***thalaji.*** ]uk.6

Thalaji inatumika kama mhimili na inadhihirisha uwezo wa kifedha na utajiri wa familia ya Bw. Mambo. Hii ni kwa sababu kwa wengi, kupata thalaji huwa ni kitu adimu na hufungamanishwa na watu walio na fedha na uwezo mkubwa wa kiuchumi.

Mihimili pia inapatikana katika onyesho la pili.

**21.** [*Ukumbini pale pale. Fatuma na Bi. Sikitu wanaweka vyakula mezani. Bwana Mambo aliyevaa* ***miwani*** *amekaa katika* ***sofa*** *anasoma* ***gazeti..***.] uk 15

Katika onyesha hili vifaa kama vile miwani, sofa na gazeti vimetumika kama mihimili. Vifaa hivi bado vinabainisha kuwa kwa kweli, familia ya Bw. Mambo ni familia iliyojiweza kiuchumi. Katika onyesho hili vile vile, Faki na Fikirini wanaonekana wakisoma kitabu kilichoandikwa na Mwandishi Zanga. kitabu hiki kinatumika kama mihimili kuonyesha jinsi marafiki hawa walivyopenda kusoma, kuhakiki na kuchambua vitabu vya fasihi.

**22.** FAKI: [ *Kwa sauti ya chini na huku amekamata kitabu cha mwandishi* ***zanga***] uk 15.

**Hitimisho**

Kwa msingi wa madhumuni na nadharia iliyoongoza utafiti huu, imebainika katika utafiti huu kuwa katika kuangazia vipengele vya utendaji, huna budi kugusia namna vinachangia na kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa tamthilia jukwaani na kuusukuma mchezo mbele. Mtafiti ametaja kwa ufupi ujumbe ambao umefungamana na vipengele vya utendaji, suala ambalo linakubaliana na maoni ya Williams (1968) ya umuhimu wa kuchunguza uhusiano uliopo kati ya matini na utendaji. Imebainika ya kwamba tendo la kidrama hufungamana na usemi wa kidrama. Tamthilia ya *Kitumbua Kimeingia Mchanga* inaweza kudai nafasi kama matini za kidrama. Hii ni kwa sababu, katika kuitathmini tamthilia hii mtafiti alibaini kuwa mtunzi wake amevitumia vipengele vya utendaji kwa kiwango cha juu sana katika kufanikisha ujumbe wake. Isitoshe, imebainika waziwazi kuwa maelekezo ya jukwaa yamebuniwa kulingana na mahitaji ya uigizaji na kuusogeza mchezo mbele. Vipengele vya utendaji vilivyobainika ni kama vile maelezo ya jukwaa, sauti, mwangaza, mandhari, maleba na mihimili. Mtafiti anapendekeza kuwa tafiti za baadaye zifanywe kuhusu suala la matumizi ya lugha ya kidrama na dhima yake katika tamthilia za kisasa na pia nadharia ya utendaji iweze kutumiwa kuchanganua tamthilia mbalimbali za Kiswahili.

**Marejeleo**

Auslander, P. (2008). *Theory for Performance Studies. A student Guide*. London and New York: Roughtledge.

Griffiths, M. & Hemming, E. (1984). *A Sense of Dramatic Critism and Appreciation*: Britain: Collins Educational.

Madison, D. & Hamera, J. (2005). *The Sage Handbook of Perfomance of Arts and Theatre Studies*. New York: Newsbury Park.

Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: *Textbooks Graphics and Publishing*.

Mohamed, S.A. (2000). *Kitumbua Kimeingia Mchanga*. Nairobi: Oxford Press.

Wallace, B. (1984). *Theories of Performance*. New York: Rinchart and Winston.

Wamitila, K. (2003). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Litho Limited.

Wamitila. K. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.

Wamitila, K. (2011). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

Were, E. (2012). *Fani Katika Tamthilia za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi

Williams, R. (1968). *Drama in performance*. London: C.A. Watts & Co. Ltd.

Wilson, E. (1988). *The Theatre Experience.* New York: The McGraw Hill Companies.